



Ninapaswa kuleta nini wakati wa ziara yangu ya kwanza ya WIC?

Wanawake, watoto wachanga na watoto wanaotuma maombi ya kusajiliwa kwa WIC ni lazime wawepo wakati wa ziara ya kwanza. Unahitaji pia kuleta vifuatavyo:

Thibitisho la Mapato Yanayostahiki

Ikiwa unapokea MaineCare, SNAP, au TANF, ni lazima ulete vifuatavyo:

- Kadi ya MaineCare au barua ya kustahiki kwa watu wote wanaotuma maombi ya kusajiliwa kwa WIC
- Barua ya kusajiliwa kwa au kuanzisha upya kwa usajili wako kwa mpango wa SNAP
- Rekodi za usaidizi wa kifedha unaopokea kutoka kwa mpango wa TANF

Mapato ya wanafamilia wote wa boma yako ya siku 30 zilizopita. Haya yanajumuisha, lakini sio tu:

- Rekodi za kuthibitisha malipo kwa siku 30 zilizopita
- Rekodi ya malipo kutoka kwa jeshi/ Rekodi ya Mapumziko na Mapato (LES)
- Rekodi ya malipo kutoka kwa mwajiri
- Makubaliano ya usaidizi kwa mtoto au mtalikiwa
- Bima ya Ulemavu ya Huduma za Kijamii (SSDI) au rekodi ya Malipo ya Ziada kutoka kwa Serikali Kuu (SSI)

Thibitisho la mahali unapoishi (anwani halisi ya eno unaloishi, sio sanduku la posta).

Mifano ni pamoja na:

- Bili ya gharama za matumizi yenye jina lako, inayolingana na anwani uliyopeana
- Barua yenye jina na anwani yako
- Leseni ya dereva yenye anwani ya mtaa wako
- Mkataba wa upangaji au karatasi ya mkopo wa kununua nyumba wenye jina na anwani yako
- Rekodi ya malipo ya TANF, kadi ya MaineCare
- Barua ya kusajiliwa au kuanzisha upya kwa usajili wako kwa mpango wa SNAP

Thibitisho la utambulisho kwa kila mmoja anayetuma ombi la kusajiliwa kwa WIC.

Mifano inajumuisha:

- Kadi ya MaineCare
- Leseni ya dereva
- Kadi ya SSID
- Kadi ya Kitambulisho ya Shule au ya Mwajiri
- Kadi ya kitambulisho iliyotolewa na Jimbo
- Pasipoti
- Hati ya kuzaliwa
- Kadi ya hospitali yenye maelezo ya mtoto anapozaliwa
- Rekodi ya chanjo